JAMHURI YA
MUUNGANO
WA TANZANIA

**WIZARA YA
KATIBA NA
SHERIA**

Dodoma Mei, 2025




# TOLEO MAALUMU LA BAJETI 2025/26





**Dira:** Katiba na Sheria wezeshi kwa maendeleo ya Taifa.

**Dhima:** Kuwa na mfumo madhubuti wa kikatiba na kisheria wenye kufanikisha utekelezaji wa sera na mipango kwa maendeleo ya Taifa.

# Vipaumbele vya Wizara katika Mwaka wa Fedha 2025/2026

**(i)** Kuimarisha huduma za msaada wa kisheria kwa watu wenye uhitaji
**(ii)** Kushughulikia masuala ya kikatiba pamoja na kutoa elimu ya Katiba na Uraia kwa umma
**(iii)** Kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai Nchini
**(iv)** Kubainisha na kutatua migogoro ya kisheria kwa wananchi na wadau wengine;
**(v)** Kuimarisha mifumo ya utoaji haki ili haki ipatikane kwa wote na kwa wakati
**(vi)** Kuboresha mfumo wa kitaifa na kuzingatia mifumo ya kikanda na kimataifa kuhusu haki za binadamu na utawala bora
**(vii)** Kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika masuala ya haki jinai na haki madai
**(viii)** Kuwezesha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Sekta ya Sheria nchini
**(ix)** Kuimarisha mifumo kisheria na kitaasisi katika Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala
**(x)** Kuimarisha usimamizi wa mikataba ya utajiri asili na maliasilia za nchi ambazo Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zimeingia na wawekezaji
**(xi)** Kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na majadiliano ya mikataba
**(xii)** Kuimarisha mfumo wa uandishi, ufasiri na urekebu wa sheria 98
**(xiii)** Kuongeza uelewa kwa Watendaji wa Serikali na Wananchi kuhusu Sheria za Nchi
**(xiv)** Kuimarisha utafiti, tathmini na mapitio ya Sheria
**(xv)** Kuendesha mashtaka ya jinai na kuimarisha shughuli za utenganishaji wa mashtaka na upelelezi
**(xvi)** Kuimarisha uratibu, usimamizi na uwakilishi katika kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi
**(xvii)** Ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika sekta ya sheria
**(xviii)** Kusimamia na kuendeleza elimu na taaluma ya Sheria nchini
**(xix)** Kuwezesha usajili wa matukio muhimu ya binadamu na kusimamia masuala ya ufilisi na udhamini
**(xx)** Kuwezesha ajira, uteuzi, kuimarisha nidhamu na maadili ya watumishi wa Mahakama
**(xxi)** Kuimarisha mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha huduma za kisheria nchini
**(xxii)** Kuendeleza rasilimali watu katika Sekta ya Sheria




## BODI YA UHARIRI

**Ndg. Eliakim Chacha Maswi**
Katibu Mkuu

**Hyasinta Kissima**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**Wajumbe:**
Grace Gwamagobe
Pili Nashon
Brown Jonas

# WIZARA YA KATIBA NA SHERIA YAIDHINISHIWA BAJETI YA 687,698,489,000 KWA MWAKA 2025/26




Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeidhinisha jumla ya Shilingi Bilioni mia sita themanini na saba, milioni mia sita tisini na nane laki nne na themanini na tisa elfu (687,698,489,000) kama bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwaajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa mwaka ujao wa fedha 2025/26.

Awali Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas Ndumbaro aliwasilisha hotuba ya makadirio ya bajeti hiyo tarehe Aprili 30, 2025, akiomba idhini ya Bunge la Tanzania kupititisha makadirio hayo huku akiainisha vipaumbele katika mwaka huo wa fedha kuwa ni pamoja na kuimarisha huduma za msaada wa kisheria kwa wenye uhitaji pamoja na kushughulikia masuala ya Kikatiba na kutoa elimu ya Katiba na uraia kwa wananchi.

Wizara pia kwa mwaka 2025/26 imepanga kuboresha Taasisi za haki jinai, kubainisha na kutatua migogoro ya kisheria kwa wananchi, kuimarisha mifumo ya utoaji haki pamoja na kuendelea kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa katika masuala ya Haki jinai na Haki madai.

Pia Wizara imepanga kuwezesha matumizi ya kiswahili katika sekta ya sheria, kuimarisha tafiti na tathmini ya mapitio ya sheria, ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika sekta ya sheria, pamoja na kuwezesha ajira, uteuzi na kuimarisha nidhamu na maadili kwa watumishi wa mahakama sambamba na kuimairisha matumizi ya TEHAMA na uendelezaji wa Rasilimali watu ndani ya Wizara na Taasisi zake.



# HII NI BAJETI YA SHIBE KWA WENYE NJAA NA KIU YA HAKI – DKT. NDUMBARO

**"Bajeti hii sisi tunaita bajeti ya haki. Bajeti ambayo inaenda kumpa haki Mtanzania, kutoa shibe kwa Watanzania wenye njaa na kiu ya haki. Italeta mwanga na kuondoa giza la dhulma ya haki kwa Watanzania wanyonge katika kona zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Waziri wa Katiba na Sheria, Dkt. Damas Ndumbaro amesema bajeti ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni bajeti ya haki inayolenga kuwapatia Watanzania, hususan wanyonge, fursa sawa ya kupata haki katika kila kona ya nchi.

Akizungumza bungeni jijini Dodoma Aprili 30, 2025, wakati wa kuhitimisha hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya wizara hiyo, Dkt. Ndumbaro alisema bajeti hiyo inaenda kufuta machozi ya Watanzania waliodhulumiwa haki kwa muda mrefu.

"Bajeti hii sisi tunaita bajeti ya haki. Bajeti ambayo inaenda kumpa haki Mtanzania, kutoa shibe kwa Watanzania wenye njaa na kiu ya haki. Italeta mwanga na kuondoa giza la dhulma ya haki kwa Watanzania wanyonge katika kona zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alisema.

Waziri huyo ameeleza kuwa bajeti hiyo imeandaliwa kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa haki, hasa kwa wananchi wa kawaida ambao kwa miaka mingi wamekuwa wakikumbana na changamoto mbalimbali katika kupata huduma za kisheria.

# MSAADA WA KISHERIA WATAJWA KUWA MOJA KATI YA VIPAUMBELE 22 WIZARA YA KATIBA NA SHERIA



Wizara ya Katiba na Sheria imetaja vipaumbele 22 vya bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kuwa ni pamoja na Kuimarisha huduma za msaada wa kisheria kwa watu wenye uhitaji.

Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas Ndumbaro ametaja vipaumbele hivyo Aprili 30, 2025, bungeni wakati akiwasilisha hotuba ya makadirio ya bajeti ya Wizara hiyo na Taasisi zake ambapo aliliomba Bunge na likaidhinisha jumla ya shilingi bilioni 687.7.

Alitaja vipaumbele vingine kuwa ni kushughulikia masuala ya kikatiba, kutoa elimu ya Katiba na Uraia kwa umma, Kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai Nchini, Kubainisha na kutatua migogoro ya kisheria kwa wananchi na wadau wengine.

Dkt Ndumbaro ameongeza kuwa vipaumbele vingine ni pamoja na kuimarisha mifumo ya utoaji haki ili haki ipatikane kwa wote na kwa wakati, kuzingatia mifumo ya kikanda na kimataifa kuhusu haki za binadamu na utawala bora, Kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika masuala ya haki jinai na haki madai na Kuwezesha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Sekta ya Sheria nchini.

Alisema, " Wizara imejipanga Kuimarisha mifumo kisheria na kitaasisi katika Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala, Kuimarisha usimamizi wa mikataba ya utajiri asili na maliasilia za nchi ambazo Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zimeingia na wawekezaji; Kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na majadiliano ya mikataba, Kuimarisha mfumo wa uandishi, ufasiri na urekebu wa sheria 98".

Vipaumbele vingine ni pamoja na kuongeza uelewa kwa Watendaji wa Serikali na Wananchi kuhusu Sheria za Nchi, Kuimarisha utafiti, tathmini na mapitio ya sheria, Kuendesha mashtaka ya jinai na kuimarisha shughuli za utenganishaji wa mashtaka na upelelezi, Kuimarisha uratibu, usimamizi na uwakilishi katika kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi.

Dkt Ndumbaro alitaja vipaumbele vingine kuwa ni Ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika sekta ya sheria, Kusimamia na kuendeleza elimu na taaluma ya Sheria nchini, Kuwezesha usajili wa matukio muhimu ya binadamu na kusimamia masuala ya ufilisi na udhamini.

Dkt Ndumbaro alisisitiza kuwa Wizara imejipanga pia kuwezesha ajira, uteuzi, na kuimarisha nidhamu na maadili ya watumishi wa Mahakama, Kuimarisha mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha huduma za kisheria nchini na Kuendeleza rasilimali watu katika Sekta ya Sheria.

Pamoja na hayo Waziri Ndumbaro alisema katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, baadhi ya kazi zitaka-




zotekelezwa na Wizara ya Katiba na Sheria (Fungu 41) katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni pamoja na Kuandaa Sera ya Taifa ya Msaada wa Kisheria, Kutoa huduma za msaada wa kisheria ikiwemo kutekeleza Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia.

Pia Wizara itatoa elimu kwa umma kuhusu Sera ya Taifa ya Haki Jinai; Kutoa Elimu ya Uraia kwa umma na utawala bora kwa Viongozi na watendaji kwa Halmashauri 100 kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yam waka 1977.



" Kuimarisha mfumo wa usimamizi, uratibu na kuwajengea uwezo wataalam wa Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala, Kuratibu na kuwezesha Mapitio ya Sheria zinazohusu Haki jinai, Kuwezesha uandaaji wa miongozo ya ufuatiliaji wa masuala ya haki za binadamu 100 na uandishi wa taarifa za Haki za Binadamu"alisema.

Vilevile alisema Wizara itaratibu na kushiriki mikutano ya Kikanda na ya Kimataifa, Kujenga uwezo kwa wananchi kuhusu uelewa wa Sheria za Utajiri na Maliasilia za Nchini Sura 449 na 450, Kuangalia Sheria zinazodhibiti masuala ya Utajiri Asili na Maliasili kama zinakidhi matakwa ya Sheria Sura ya 449 na 450.

Dkt Ndumbaro ameongeza kuwa Wizara itafanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mfumo wa utoaji haki, Kuratibu na kusimamia usajili wa matukio muhimu ya binadamu ya vifo, ndoa, talaka na watoto wa kuasili, Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kisheria, Kuimarisha mifumo ya upatikanaji haki madai, na Kutoa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo kwa wanafunzi 1,300.

Hata hivyo katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara, Taasisi zake na Mhimili wa Mahakama inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi 13,656,199,000 ikiwa ni maduhuli.

# MSAADA WA KISHERIA WA MAMA SAMIA WAFIKIA WANANCHI 2,698,908 NA ITAKUWA ENDELEVU NCHINI




Waziri wa Katiba na Sheria nchini Tanzania Dkt. Damas Ndumbaro amesema Kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia imewafikia jumla ya wananchi 2,698, 908, kati yao wanaume wakiwa ni 1,347,325 na wanawake wakiwa 1,351,583 katika Mikoa 25 ya Tanzania bara.

Dkt. Ndumbaro amesema Kampeni hiyo imetekelezwa katika Halmashauri 179, Kata 1907, Vijiji na Mitaa 5702 vikifikiwa huku migogoro 24,691 iliyodumu kwa muda mrefu mingine kwa zaidi ya miaka kumi ikipokelewa na kutatuliwa, suala ambalo limewezesha amani, utulivu na utengamano miongoni mwa wanajamii.

"Migogoro hii ni ya ardhi, ndoa za utotoni, matunzo ya watoto, ndoa, jinai, ukatili wa kijinsia na migogoro 5704 ilitatuliwa na kuhitimishwa kwa njia mbadala kati ya migogoro 23,399 ya muda mrefu iliyopokelewa.", alisema Dkt. Ndumbaro.

Wakati wa uwasilishaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2025/26 Jumatano Aprili 30, 2025, Bungeni Dodoma, Dkt. Ndumbaro pia alieleza kuwa katika kuhakikisha kuwa msaada wa kisheria unakuwa endelevu kwa wananchi, Serikali imeanzisha madawati ya msaada wa kisheria kwenye mamlaka 184 za serikali za mitaa Tanzania bara, lengo likiwa ni kusogeza huduma na kukuza uendelevu wa msaada huo wa kisheria.

# Awamu ya Kwanza ya Kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia kuhitimishwa Juni, 2025

Waziri wa Katiba na Sheria nchini Tanzania Dkt. Damas Ndumbaro ameliambia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa kufikia Mwezi Juni Mwaka 2025 kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia itaanza rasmi kwa Mkoa wa Dar Es salaam ili kuhitimisha mikoa yote ya Tanzania bara na Zanzibar.

Dkt. Ndumbaro ameeleza hayo wakati akiwasilisha hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2025/26 Jumatano Aprili 30, 2025 Bungeni Dodoma na kuongeza kuwa Wizara bado inaendelea na uratibu na utekelezaji wa Kampeni hiyo.

"Tangu kuanza kwa kampeni hii tarehe 27, mwezi wa nne mwaka 2023 kampeni hii tayari imefanyika kwenye mikoa ya Dodoma, Manyara, Shinyanga, Ruvuma, Simiyu, Singida, Iringa, Mara. Songwe, Morogoro, Njombe, Katavi, Tabora, Geita, Kigoma, Mtwara, Mwanza, Kilimanjaro, Mbeya, Lindi, Rukwa, Pwani, Arusha, Tanga na Kagera.",aliongeza Dkt. Ndumbaro.

Katika hatua nyingine, Dkt. Ndumbaro ameelezea utekelezaji wa kampeni hiyo kwa upande wa Zanzibar, akieleza kuwa kampeni hiyo tayari imetekelezwa kwenye mikoa ya Kaskazini Pemba, Mjini Magharibi na Kaskazini Unguja na kwasasa inatekelezwa mwenye mikoa ya Kusini Pemba na Kusini Unguja huku ikitarajiwa kukamilika Mwezi Mei mwaka Mei 2025.

Wakati huo huo Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro ameliambia Bunge la Tanzania na watanzania kwa ujumla kuwa Kutokana na maelekezo mahususi ya Rais Samia Suluhu Hassan na utekelezaji wa sheria ya msaada wa kisheria kwa wananchi, Kampeni ya Msaada wa kisheria ya Mama Samia haitokufa- itakuwa endelevu, ikitarajiwa kuzinduliwa awamu ya Pili mwezi Juni mwaka huu.

Dkt. Ndumbaro ameongeza kuwa tayari wizara imeanzisha madawati ya msaada wa kisheria kwenye Halmashauri zote 184 nchini huku ikiingia makubaliano na Chama Cha wanasheria wa Tanganyika TLS, Asasi za kiraia zenye kushughulika na masuala ya kisheria pamoja na Vyuo vikuu nchini kwaajili ya kuendelea kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi.

Amesema Kampeni hiyo iliyoasisiwa na kufadhiliwa na Rais Samia ni sehemu ya Utekelezaji wa sheria ya Bunge, ahadi ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 pamoja na utekelezaji wa Maagizo na maelekezo mahususi ya Rais Samia, wakati alipokutana na Waziri huyo na kumueleza kuhusu uanzishwaji wake.

Dkt. Ndumbaro pia ameahidi kuchukua ushauri wa Wabunge mbalimbali waliochangia, wakitaka kuanzishwa kwa mfuko wa Msaada wa kisheria (Legal Aid Fund) kwaajili ya kusaidia utekelezaji wa programu hiyo yenye kutoa msaada wa kisheria kwa watu wa pembezoni na wenye uchumi mdogo ili waweze kugharamia huduma za kisheria.





# ‘2024 tumefanya mabadiliko makubwa zaidi ya Sheria na Mifumo ya Uchaguzi’

Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas Ndumbaro amesema katika Historia ya Tanzania, mwaka 2024 kumefanyika mabadiliko makubwa ya sheria na mifumo ya uchaguzi kupitia Bunge la Tanzania, ikiwezesha pia kupatikana kwa Tume huru ya Taifa ya Uchaguzi.

“Baada ya majadiliano ya muda mrefu na yenye kushirikisha pande zote, Februari mwaka 2024 ndipo tulipofuta sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya mwaka 1985 na kutunga sheria mpya ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani yenye vifungu 168.Ukitaja kujua Uhuru wa Tume ya uchaguzi ya sasa nenda kasome sheria hii ya Uchaguzi.”, aliongeza Dkt. Ndumbaro.

Dkt. Ndumbaro alieleza kushangazwa na kauli za No Reforms, No Election zilizotajwa na baadhi ya Wabunge, kutoka kwa wanaodai mabadiliko ilihali tayari mabadiliko yamefanyika mwaka jana kwa kutungwa kwa sheria hiyo mpya ambayo bado haijatumika, ikisubiri kutumika kwake kwa mara ya kwanza katika uchaguzi Mkuu wa Mwezi Oktoba 2025.

Dkt. Ndumbaro pia alifafanua kuwa hadi sasa sheria za uchaguzi zimefanyiwa marekebisho makubwa mara 15 ambapo awali katika uchaguzi wa mwaka 1958 na 1959 uchaguzi uliegemea katika ubaguzi wa rangi, baadae 1962 yakafanyika mabadiliko, 1995 ukaanza mfumo wa vyama vingi na sasa imetungwa sheria ya Taifa ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2024.

Aidha Dkt. Ndumbaro ameeleza kuwa kanuni za maadili ya uchaguzi wa mwaka 2025 zimeshatungwa na vyama vyote vya siasa vimeshasaini kanuni hizo isipokuwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo Chadema ambacho kwa utashi wake binafsi na bila kulazimishwa kimeamua kutosaini kanuni hizo.

# MAHAKAMANI NA BUNGENI NDIPO KUNAPOFANYIKA MABADILIKO SIO BARABARANI – DKT. NDUMBARO

Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas Ndumbaro amesema suala la Upatikanaji wa Mwenyekiti wa Tume huru ya Taifa ya Uchaguzi, Mkurugenzi wa uchaguzi na Maafisa wengine wa Juu wa Tume huru ya Taifa ya Uchaguzi litatangazwa ili watu wenye sifa waweza kuomba, kufanyiwa usahili na baadae kuidhinishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Dkt. Ndumbaro alisema mchakato huo utasimamiwa na Kamati ya usaili ambayo itaanzishwa ikijumuisha Wajumbe watano ambao ni Majaji Wakuu wa Tanzania na Zanzibar, Mwenyekiti na Makamu mwenyekiti wa Tume ya haki za binadamu na utawala bora pamoja na mtu mmoja atakayeteuliwa baadae ili kukamilisha idadi ya watu watano watakaosimamia mchakato wa upatikanaji wa Maafisa wa juu wa Tume huru ya Taifa ya Uchaguzi.

Katika maelezo yake wakati akijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa wakati wa mjadala wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria Aprili 30, 2025, Dkt. Ndumbaro ameeleza kuwa duniani kote taratibu za namna hiyo huwa ni za aina tatu, Rais achague mwenyewe, Bunge lichague na baadae kuidhinishwa na Rais ama Kiundwe chombo maalum cha kufanya hivyo kama ambavyo Tanzania imeamua ili kuwa na Tume huru kweli itakayosimamia mchakato wa uchaguzi.

Dkt. Ndumbaro pia amezungumzia suala la Wakurugenzi wa Halmashauri kusimamia chaguzi, akieleza kuwa kupitia sheria mpya ya uchaguzi ya mwaka 2024, Wakurugenzi hao hawatasimamia tena na badala yake Maafisa maandamizi wa serikali watakaopatikana kwa njia ya ushindani ndiyo watakaosimamia uchaguzi huo.

Aidha ameeleza kuwa sheria ya sasa imepiga marufuku mtu kupita bila kupingwa, kikiwa ni kilio cha muda mrefu kilichowahi kufikishwa mpaka mahakamani na Mahakama ikatoa maamuzi ambayo sasa yameingizwa rasmi katika sheria ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani.

“Hili lilikuwa lalamiko kubwa sana mpaka watu walienda mahakamani, mahakama ikatoa hukumu, hukumu ya mahakama imetekelezwa na hii tunajifunza hapa kwamba kumbe tukitaka mabadiliko twende Bungeni ama twende mahakamani na sio kulazimisha watu kuingia mtaani au barabarani.” aliongeza.



# NAIBU SPIKA ZUNGU AVIITA VYAMA VYA UPINZANI KUSHIRIKI UCHAGUZI 2025

## ■ Sheria ya sasa ni bora kuliko ile iliyowapa ushindi 2015



Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mussa Azzan Zungu, ameviita Vyama vya Upinzani nchini Tanzania kushiriki katika Uchaguzi Mkuu wa baadae mwaka huu, akieleza kuwa hata mabadiliko wanayoyataka na kuyahimiza ya kisheria na kimfumo yatapatikana ndani ya Bunge hilo na sio barabarani.

Naibu Spika amebainisha hayo Jioni ya Aprili 30, 2025 wakati akiishukuru Wizara ya Katiba na Sheria kwa hotuba ya Bajeti waliyoiwasilisha mapema Asubuhi pamoja na hitimisho la mjadala wa hotuba hiyo walioufanya, akieleza kuwa kwasasa Tume ya Uchaguzi ni bora zaidi kuliko ile ambayo ilifanikisha Bunge kuwa na Waheshimiwa wabunge wa Vyama pinzani takribani 112 kutoka vyama mbalimbali.

Akimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kujivua madaraka aliyokuwa nayo awali kwenye uteuzi wa Viongozi mbalimbali wanaosimamia uchaguzi Mkuu, Naibu Spika amesisitiza kwa wizara pia umuhimu wa kwenda kuwaeleza wananchi mabadiliko mbalimbali ya sheria za uchaguzi yaliyofanyika sambamba na ushiriki wa Vyama vya upinzani ulivyokuwa wakati wa mchakato wa mabadiliko hayo yaliyofanywa na Bunge na mamlaka nyingine mbalimbali.

Naibu Spika Zungu akieleza maagizo yake kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Bwana Eliakim Maswi, ameeleza pia umuhimu wa kutumia mitandao ya kijamii katika kuelimisha na kuufahamisha umma kuhusu mabadiliko hayo ili kuwafanya wananchi kuujua ukweli na kuukataa upotoshaji mkubwa unaoendelea katika mitandao ya Kijamii kutoka kwa baadhi ya Wanasiasa na vyama vya siasa nchini.



# Rasimu Sera ya Taifa ya Jinai kuidhinishwa rasmi Mwaka ujao wa Fedha

Wizara ya Katiba na Sheria nchini Tanzania imeandaa Rasimu ya sera ya Taifa ya Jinai na Mkakati wa utekelezaji wa sera hiyo ambapo kulingana na Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas Ndumbaro, Sera hiyo inatarajiwa kuidhinishwa na serikali katika mwaka ujao wa serikali 2025/26.

Jumatano Aprili 30, 2025, Bungeni Mjini Dodoma, wakati wa uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, Dkt. Ndumbaro ameliambia Bunge kuwa lengo la Sera hiyo ni kuhakikisha kuwa kunakuwepo na mfumo Jumuishi utakaokuwa unashughulikia masuala ya Haki jinai.

Katika hatua nyingine, Dkt. Ndumbaro akieleza programu mbalimbali zilizotekelezwa na Wizara yake kwa mwaka 2024/25, alisema Wizara hiyo pia imetoa mafunzo ya elimu ya uraia na utawala bora kwa wajumbe wa Kamati za usalama za Mikoa na Wilaya, watendaji wa Kata, Menejimenti na wataalamu wa Halmashauri zipatazo 122 katika Mikoa 17 ya Tanzania bara.

Aidha akizungumzia mkakati wa ujenzi wa kizazi chenye uzalendo, maadili na uwajibikaji, alisema kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI na wizara ya Elimu, waliandaa maudhui ya Katiba na Uraia kwa shule za msingi, sekondari na vyuo vya mafunzo ya ufundi kote Tanzania bara.

> **“ Wizara pia imetoa mafunzo ya elimu ya uraia na utawala bora kwa wajumbe wa Kamati za usalama za Mikoa na Wilaya, watendaji wa Kata, Menejimenti na wataalamu wa Halmashauri zipatazo 122 katika Mikoa 17 ya Tanzania bara.**

# Toleo la Pili la Urekebu wa Sheria Kuu za Nchi la Mwaka 2023 kuanza kutumika Julai Mosi, 2025



Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas Ndumbaro amelieleza Bunge la Tanzania kuwa Wizara hiyo kupitia kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali imeendelea kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinaenda na wakati na zina akisi sera na vipaumbele vya serikali katika nyanja zote za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kuitamaduni, mazingira na kiteknolojia.

Katika kutekeleza hilo, Dkt. Ndumbaro aliyekuwa akiwasilisha hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na sheria kwa mwaka 2025/26 ameeleza kuwa Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali iliandaa miswada ya sheria 16 pamoja na kuhakiki na kupitisha sheria ndogo 903, kulinganisha na sheria ndogo 885 zilizopitishwa katika kipindi cha Julai - Aprili mwaka 2023/24.

Dkt. Ndumbaro pia amefafanua kuwa Wizara imekamilisha urekebu wa sheria kuu 446 na kuandaa toleo la nchi la sheria zilizofanyiwa urekebu la mwaka 2023, likiwa ni toleo la pili tangu kupatikana kwa uhuru, toleo la kwanza likiwa la mwaka 2002, lililokuwa limefadhiliwa na Benki ya dunia na Toleo hili la pili limeandaliwa kwa fedha za ndani na wataalamu wa ndani, likitarajiwa kuanza kutumika rasmi Julai Mosi 2025 mara baada ya kuzinduliwa na Rais Samia mnamo Aprili, 23, 2025.



# Kazi zitakazotekelezwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali



**OFISI ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 itatekeleza kazi zifuatazo Kuimarisha Usimamizi na Ufuatiliaji wa Mikataba iliyosainiwa na kuingiwa na Serikali; na Kutoa elimu ya kisheria kwa jamii kupitia Kliniki za Sheria ili kuwaongezea uelewa wananchi kuhusu wajibu na haki zao. (**

Kuboresha mifumo ya TEHAMA na kuimarisha matumizi yake katika utoaji wa huduma za kisheria, Ujenzi wa majengo ya Ofisi za Vituo Jumuishi vya Taasisi za Serikali za Kisheria Nchini katika mikoa ya Mtwara na Tabora.

### Kazi zitakazo tekelezwa na Ofisi ya Wakili Mkuu.

- **Mashauri ya madai 9013 yameendeshwa**

KATIKA kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendesha jumla ya mashauri ya Madai 9,013.

> **Kwa kumalizika kwa mashauri hayo, Ofisi imefanikiwa kushinda mashauri 750 sawa na asilimia 77.6% ya mashauri yaliyomalizika.**

Hayo aliyasema jana Bungeni Dkt. Damas Ndumbaro ambapo alisema kuwa kati ya Mashauri hayo, Mashauri 8,347 ni madai ya kitaifa, Mashauri 33 ni ya madai ya kimataifa na mashauri 633 ni mashauri ya Kikatiba na Haki za Binadamu.

Alisema katika kuendesha mashauri hayo, mashauri 966 yalimalizika. Kati ya mashauri yaliyomalizika, mashauri 814 ni ya madai ya kitaifa, shauri moja ni la madai ya kimataifa na mashauri 151 ni ya Kikatiba na Haki za Binadamu.

"Kwa kumalizika kwa mashauri hayo, Ofisi imefanikiwa kushinda mashauri 750 sawa na asilimia 77.6% ya mashauri yaliyomalizika kwa 44 kipindi husika na kuokoa kiasi cha Shilingi 51,022,810,719.81 kiasi ambacho Serikali ingelipa endapo ingeshindwa mashauri hayo,"alisema.

Aidha alitaja baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni pamoja na Kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri ya Madai na Usuluhishi yaliyopo na yatakayofunguliwa na au dhidi ya Serikali na Taasisi zake.

Kuanzisha Ujenzi wa ofisi za Wakili Mkuu wa Ser-

ikali katika mikoa iliyo na Masjala za Mahakama Kuu, Kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa mashauri ili kuwa na mfumo thabiti katika kukusanya, kuhifadhi na kutoa taarifa sahihi na Kuboresha ufanisi na utendaji kazi kwa kununua vitendea kazi na kutoa mafunzo kwa watumishi.

## Kazi zitakazotekelezwa na Ofisi ya Mashtaka

- **Kesi kubwa 177ziliendeshwa**

KATIKA mwaka 2024/2025 hadi Aprili, 2025, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha kesi kubwa 177 katika Mahakama Kuu – Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ikilinganishwa na kesi 60 zilizoendeshwa kipindi kama hicho mwaka 2023/2024.

Akizungumza jana Bungeni Dkt. Damas Ndumbaro alisema katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili, 2025, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha jumla ya kesi 2,638 katika Mahakama Kuu ya Tanzania ikilinganishwa na kesi 6,409 zilizoendeshwa katika kipindi kama hicho mwaka 023/2024.

Aidha, kesi 108 sawa na asilimia 61 zilihitimishwa ikilinganishwa na kesi 22 zilizohitimishwa katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 na kesi 69 sawa na asilimia 38 zinaendelea katika hatua mbalimbali.

Pamoja na hayo alitaja baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni pamoja na Kuendelea na uendeshaji wa kesi za jinai Kufanya ukaguzi katika maeneo yanayohifadhi mahabusi na wafungwa.

**177**

**Idadi ya kesi kubwa zilizoendeshwa mwaka 2024/2025 hadi Aprili, 2025 na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika Mahakama Kuu – Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ikilinganishwa na kesi 60 zilizoendeshwa kipindi kama hicho mwaka 2023/2024.**

Pia kuendesha mashauri ya utaifishaji wa mali zinazotokana na uhalifu; na Kuendelea na ujenzi wa Majengo ya Ofisi za Mashtaka katika Mikoa na Wilaya. 103 175.

## Kazi zitakazotekelezwa na mfuko wa Mahakama

KAZI zitakazotekelezwa na Mfuko wa Mahakama katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni pamoja na Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu (Backlog);

Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama,Kuendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mahakama,Kuboresha mifumo ya Teknolojia ya Habari na





Mawasiliano (TEHAMA).

Kuimarisha na kuboresha huduma za mafunzo endelevu ya kimahakama na sheria kwa watumishi wa mahakama na wadau wengine.

## Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

### THBUB yasajili malalamiko mapya 160

WIZARA kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeendelea kupokea na kushughulikia malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Hayo aliyasema jana Bungeni Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas Ndumbaro wakati alipokuwa akiwasilisha Bungeni Makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake ambapo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Alisema katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 THBUB ilianza na malalamiko 759 na kusajili malalamiko mapya 160 kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 hivyo kufanya jumla ya malalamiko hayo kuwa 919.

> **Kazi zitakazotekelezwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni pamoja na Kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora katika Mikoa 26 ya Tanzania bara na Mikoa mitano ya Zanzibar.**

Pamoja na hayo alitaja kazi zitakazotekelezwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni pamoja na Kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora katika Mikoa 26 ya Tanzania bara na Mikoa mitano ya Zanzibar.

Kushughulikia malalamiko ya uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na kufanya ufuatiliaji wa 104 mapendekezo ya THBUB yaliyowasilishwa kwenye Taasisi za umma na binafsi.

Kufanya ukaguzi wa maeneo walimozuiliwa watu kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Magereza, Vituo vya Polisi, Mahabusu za Watoto, na vyuo vya mafunzo) na Kufanya ufuatiliaji, utafiti na tathmini ya hali ya haki za binadamu na utawala bora nchini.

## Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania.

TUME ya Kurekebisha Sheria Tanzania katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 baadhi ya kazi itakazofanya ni pamoja na Kufanya utafiti wa mfumo wa sheria zinazosimamia usajili wa Mawakili wa Kujitegemea Tanzania.

Kufanya utafiti wa mfumo wa sheria zinazosimamia biashara ya hewa ukaa (carbon trading), Kufanya utafiti utakaowezesha kutungwa kwa sheria ya matumizi ya akili unde (AI), Kufanya utafiti wa mfumo wa sheria zinazosimamia mfumo wa kupinga maamuzi ya kiutawala nchini.



Kufanya Tathmini ya Utekelezaji wa Sheria za Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki wa Utajiri Asili na Maliasili za Nchi, Sura ya 449 na sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu 105 Masharti Hasi katika Mikataba ya Utajiri Asili na Maliasilia za Nchi, Sura ya 450, Kufanya mapitio ya mfumo wa sheria za bima za magari.

Kufanya mapitio ya Sheria ya Afya na Usalama Mahala pa Kazi, Sura ya 297,Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sheria ya Ugaidi, Sura ya 19,Kuendelea na utoaji wa elimu ya sheria na kusambaza taarifa za sheria kwa umma kwa kupanua wigo wa utoaji wa huduma hiyo ili kuwafikia wananchi na wadau wa sheria wengi zaidi nchini; na Kujenga uwezo wa Watumishi kwa kuanza utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo wa Taasisi wa mwaka 2025/26 – 2029/30.



**"Kutoa mafunzo kwa Watumishi katika maeneo ya kimkakati ili kuhakikisha kunakuwa na wataalam wa kutosha na wenye ujuzi katika nyanja mbalimbali za uandishi wa sheria; na (v) Kuongeza uelewa wa Wananchi kuhusu Sheria kwa kukamilisha tafsiri ya Sheria Kuu 446 na kuanza kutafsiri Sheria Ndogo 900**

### Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria

Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni pamoja na Kuandaa Miswada ya Sheria 10, Sheria Ndogo 1,200 na Kutengeneza Sheria Ndogo Kifani 20.

Kuandaa Toleo la Urekebu wa Sheria Ndogo la Mwaka 2025 na Toleo la Urekebu wa Sheria za Afrika Mashariki la Mwaka 2025. Kuboresha/kuimarisha Mifumo ya TEHAMA 106 na matumizi yake katika Uandishi, Ufasiri na Urekebu wa Sheria hususan kujenga Mfumo wa e-Drafting, e-Translation, na eLibrary.

Vilevile Kutoa mafunzo kwa Watumishi katika maeneo ya kimkakati ili kuhakikisha kunakuwa na wataalam wa kutosha na wenye ujuzi katika nyanja mbalimbali za uandishi wa sheria; na (v) Kuongeza uelewa wa Wananchi kuhusu Sheria kwa kukamilia tafsiri ya Sheria Kuu 446 na kuanza kutafsiri Sheria Ndogo 900.




# UFANISI MKUBWA USIKILIZWAJI KESI OFISI YA TAIFA YA MASHTAKA - DKT NDUMBARO

Imeelezwa kuwa katika Kipindi cha Julai 2023 mpaka Aprili 2025, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali iliendesha kesi kubwa 177 katika Mahakama kuu Divisheni ya rushwa na uhujumu uchumi kulinganisha na Kesi 60 pekee zilizosikilizwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24.

Takwimu hizo zimebainishwa na Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt Damas Ndumbaro wakati akiwasilisha Bungeni Hotuba ya Bajeti ya Wizara yake kwa mwaka 2025/26 Jumatano Aprili 30, 2025, akieleza kwamba kesi 108 zilihitimishwa kulinganisha na Kesi 22 zilizohitimishwa kwa kipindi kama hicho cha Julai-Aprili mwaka 2023/24.

Waziri Ndumbaro pia amebainisha kuwa katika Kipindi cha Julai- Aprili mwaka 2024/25, kesi za jinai 27,523 ziliendeshwa katika mahakama za wilaya na Hakimu Mkazi kulinganisha na kesi 25,037 zilizoendeshwa katika Mahakama hizo kwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2023/24 huku pia kesi 21,232 sawa na asilimia 77 zikihitimishwa ikilinganishwa na kesi 15,084 ya kesi za mwaka 2023/24.

Wizara ya Katiba na sheria kupitia Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali imeendelea pia kusogeza huduma kwa wananchi ngazi za Mikoa na Wilaya, ambapo katika kipindi cha 2024/25 huduma hizo zimepelekwa kwenye mikoa 30 ya kimashtaka, Kwenye ofisi 108 za Wilaya huku pia Ofisi ya Mwendesha mashtaka ikikamilisha majengo yake ya Kimkoa katika mikoa ya Manyara, Shinyanga, Katavi na Rukwa.

> **Katika Kipindi cha Julai- Aprili mwaka 2024/25, kesi za jinai 27,523 ziliendeshwa katika mahakama za wilaya na Hakimu Mkazi kulinganisha na kesi 25,037 zilizoendeshwa katika Mahakama hizo kwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2023/24 huku pia kesi 21,232 sawa na asilimia 77 zikihitimishwa ikilinganishwa na kesi 15,084 ya kesi za mwaka 2023/24.**

# SERIKALI YAONGEZA KASI UTENDAJI WA MAHAKAMA KUONDOA MRUNDIKANO WA MASHAURI




Katika kuongeza kasi kwa Utendaji wa Mahakama nchini na kupunguza mrundikano wa mashauri mahakamani, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2024/25, imeongeza idadi ya watendaji mbalimbali wa Mahakama ikiwemo Majaji kumi na na Mahakimu 91, hivyo kufikisha Jumla ya Majaji 146 na Mahakimu 1426.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas Ndumbaro Jumatano Aprili 30, 2025 Bungeni Jijini Dodoma wakati akiwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara yake kwa mwaka 2025/26 huku akieleza kuwa kupunguza mrundikano wa mashauri mahakamani ni moja ya vipaumbele muhimu vya serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata haki kwa wakati.

"Katika kipindi cha Julai Mwaka 2024 hadi Aprili Mwaka 2025 kulikuwa na jumla ya mashauri takribani 238,154 mahakamani, Kati ya hayo mashauri 63, 050 yalikuwepo mwanzoni mwa Julai 2024 na mashauri 175, 104 yalifunguliwa." Ameeleza Waziri Damas Ndumbaro.

Dkt. Ndumbaro pia ameeleza kuwa kati ya mashauri 238,154 yaliyokuwepo, mashauri 174,581 yalisikilizwa na kuhitimishwa na mashauri 63,573 yanaendelea katika hatua mbalimbali huku mashauri yenye umri mrefu mahakamani yakiwa ni 2,780 sawa na asilimia 4 ya mashauri yote yaliyobakia kwenye mahakama mbalimbali za nchini Tanzania.

"Kati ya mashauri yenye muda mrefu yaliyopo mahakamani, mashauri 1,325 yapo mahakama ya rufani, 189 yapo mahakama kuu divisheni ya Makosa ya rushwa na uhujumu uchumi. Jumla ya mashauri 59 yalibakia mwishoni mwa Juni 2024, 118 yalisajiliwa, 108 yalisikilizwa na 69 yalibakia."

Pia alieleza kuwa Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 serikali imeendelea na ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama ambapo ukarabati wa Jengo la Mahakama kuu Dodoma na Iringa, Ujenzi wa vituo jumuishi vya utoaji haki kwenye Mikoa 9 pamoja na maendeleo ya ujenzi wa Mahakama za Wilaya 11 na mahakama za mwanzo 72 katika mikoa mbalimbali unaendelea.



# SERIKALI YATOA KIBALI KUAJIRI WATUMISHI 1044 SEKTA YA MAHAKAMA –SAGINI

Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini ameishukuru Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa vibali vya ajira kwa sekta ya Mahakama nchini, akishukuru kwa Vibali vya ajira 522 vilivyotolewa mwaka jana na vibali Vingine 1044 vilivyotolewa mwaka huu.

> **Wizara imeendelea pia kushughulikia uchakavu wa miundombinu ya mahakama kutokana na uwepo wa mahakama za Mwanzo na Mahakama za wilaya zilizokuwa zimejengwa tangu enzi za Mkoloni.**

Mhe. Sagini alibainisha hayo Jioni ya Aprili 30, 2025 wakati wa kuhitimisha mjadala wa Hotuba ya makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2025/26, akieleza kuwa Wizara imeendelea pia kushughulikia uchakavu wa miundombinu ya mahakama kutokana na uwepo wa mahakama za Mwanzo na Mahakama za wilaya zilizokuwa zimejengwa tangu enzi za Mkoloni.

Aidha Naibu Waziri Sagini ameeleza kuwa Wizara imepokea ushauri wa wabunge walioshauri Wizara na sekta ya mahakama kuwekeza nguvu katika ujenzi wa Mahakama kwenye ngazi za Tarafa kwa dhumuni la kuhakikisha Tarafa zote zinakuwa na Mahakama kabla ya kuhamia ngazi ya Kata.

Mhe. Sagini pia alieleza kuwa Wizara ya Katiba na Sheria inaendelea na uimarishaji wa Miundombinu ya Mahakama kuu na Mahakama Jumuishi ngazi za Mikoa, akieleza pia kuhusu Ujenzi wa mahakama ngazi ya wilaya unaoendelea kwasasa kwenye Wilaya 72 kwamba Wilaya za Ileje na Kiteto zitajumuishwa katika Mpango huo.



# WAZIRI NDUMBARO ATOA RAI KWA WAZAZI NA WAFUNGISHA NDOA KUTOA ELIMU YA MAADILI KWA WANANDOA

Waziri wa Katiba na Sheria Dkt Damas Ndumbaro ametoa wito kwa viongozi wote waliopewa dhamana ya kufungisha ndoa, wazazi na walezi kuendelea kutoa elimu ya maadili kwa wanandoa ili kupunguza talaka.

Dkt Ndumbaro ametoa wito huo Bungeni Dodoma jana wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka 2025/2026 ambapo aliliomba Bunge na liliidhinisha jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 687.7.

Aliongeza kwa kutoa wito pia kwa wanandoa kujenga utamaduni wa kuvumiliana na kutatua changamoto zinazojitokeza kwa njia ya majadiliano ili kupunguza talaka zinazoathiri malezi ya watoto kwa mustakabali wa haki zao.



Dkt Ndumbaro alieleza kuwa Wizara kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 imesajili na kutoa vyeti 675 vya talaka sawa na asilimia 116 ya lengo la kusajili talaka 583.

Alisema katika kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Kulinda Maadili, Haki na Ukatili Dhidi ya Watoto, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 RITA imesajili na kutoa vyeti 29 vya kuasili watoto sawa na asilimia 79 ya lengo la kusajili watoto wa kuasili 37.

Pamoja na hayo Dkt Ndumbaro amefafanua kuwa Wizara kupitia RITA imeendelea kuimarisha upatikanaji haki kwa wakati kwa wananchi hususan katika masuala ya mirathi ambapo katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 RITA ilipokea mashauri mapya ya mirathi 14 na kufanya jumla ya mirathi inayosimamiwa kufikia 140.

Alisema katika kipindi husika mirathi sita imefungwa baada ya kugawa mali kwa wanufaika na 134 inaendelea kufanyiwa kazi.

"Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Wakala umeandika na kutunza wosia 109 na kuendelea kutoa elimu zaidi kwa wanachi kuhusu faida za kuandika na kuhifadhi wosia ili kupunguza migogoro ya mirathi inayojitokeza katika jamii"alisema.

Aidha, RITA imetoa elimu kuhusu uandishi wa wosia na masuala ya mirathi kwa wananchi 10,858 (wanawake 6,063 na wanaume 4,795) kupitia makongamano na maonesho ya Kitaifa ikiwemo Wiki ya Sheria, Nanenane, Sabasaba na Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia katika mikoa ya Kigoma, Katavi, Rukwa, Geita na Lindi.

Pamoja na hayo alitaja baadhi ya vipaumbele vya Wizara hiyo kuwa ni pamoja na Kuimarisha huduma za msaada wa kisheria kwa watu wenye uhitaji, Kushughulikia masuala ya kikatiba pamoja na kutoa elimu ya Katiba na Uraia kwa umma.

Vipaumbele vingine vilivyotajwa na Dkt Ndumbaro ni pamoja na Kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai Nchini; Kubainisha na kutatua migogoro ya kisheria kwa wananchi na wadau wengine.

" Wizara imejipanga Kuimarisha mifumo ya utoaji haki ili haki ipatikane kwa wote na kwa wakati, Kuboresha mfumo wa kitaifa na kuzingatia mifumo ya kikanda na kimataifa kuhusu haki za binadamu na utawala bora, Kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika masuala ya haki jinai na haki madai na Kuwezesha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Sekta ya Sheria nchini", ameongeza Dkt Ndumbaro.


# Waziri Ndumbaro asifu umahiri Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia

Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas Ndumbaro amempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake mahiri na uchapakazi wake, uliosababisha mafanikio mbalimbali katika sekta tofauti ikiwemo kwenye sekta ya Sheria nchini kwa kipindi cha miaka minne ya uongozi wake.

Akitoa salamu mbalimbali wakati akiwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Sheria na Katiba kwa mwaka 2025/26 Jumatano Aprili 30, 2025 Bungeni Jijini Dodoma, Dkt. Ndumbaro amempongeza Rais Samia kwa kuteuliwa na kupitishwa na Chama Cha Mapinduzi kuwa Mgombea pekee wa Urais kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa mwaka 2025 akiambatana na Mgombea mwenza Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi ambaye kwasasa ni Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi.




Kadhalika Dkt. Ndumbaro ametoa Shukrani kwa Makamu wa Rais Dkt. Philip Isdor Mpango, Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa na Naibu Waziri Mkuu Dkt. Doto Biteko, kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakiutoa katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara ya Katiba na Sheria nchini.







*Naibu Waziri*
*Jumanne Sagini*



*Katibu Mkuu*
*Eliakim Maswi*



*Naibu Katibu Mkuu*
*Dkt. Franklin Rwezimula*

# TUNAWASHUKURU SANA KWA KUFANIKISHA VYEMA UTEKELEZAJI MAJUKUMU YA WIZARA – DKT. NDUMBARO

Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt Damas Ndumbaro ametoa shukrani kwa wadau na washirika mbalimbali wa maendeleo ikiwemo mashirika mbalimbali yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Ulaya kwa ushirikiano wao mkubwa na msaada wa kiufundi na kifedha katika kufanikisha shughuli mbalimbali za Wizara hiyo.

Dkt. Ndumbaro kadhalika amewashukuru wasaidizi wake katika Wizara wakiongozwa na Naibu Waziri Mhe. Jumanne Sagini, Katibu Mkuu Ndugu Eliakim Maswi, Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Juma, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Hamza Johari pamoja na watendaji wengine wa Wizara na Taasisi zake mbalimbali kwa namna ambavyo wamekuwa na mchango mkubwa katika kuhakikisha malengo yanafikiwa.

Wakati wa uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2025/26, Waziri Ndumbaro ametumia sehemu ya Hotuba yake pia kutoa shukrani na Pongezi kwa ushiriki wa wananchi wa Tanzania katika kutii na kuheshimu Katiba na sheria za nchi.

## Kituo cha Huduma kwa Mteja

**0262 160 360**

**Kwa malalamiko, Maswali au Ushauri unaohusiana na masuala ya kisheria.**



## Usajili wa Mashirika yanayotoa msaada wa kisheria

Tembelea Tovuti ya Wizara ya Katiba na Sheria; www.sheria.go.tz kisha bonyeza eneo la Huduma Mtandao, kisha chagua usajili wa watoa huduma za Msaada wa Kisheria. AU
Ingia moja kwa moja kwenye anuani ya https://legalaid.sheria.go.tz Nenda sehemu ya iliyoandikwa REGISTRATION kisha tengeneza akaunti ya shirika kisha fuata maelekezo kusajili shirika



# MASWI NI KATIBU MKUU BORA KABISA KATI YA NILIOWAHI KUFANYA NAO KAZI – NDUMBARO

Waziri wa Katiba na Sheria Nchini Tanzania Dkt. Damas Ndumbaro amemtaja Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndugu Eliakimu Chacha Maswi kama miongoni mwa Makatibu wake bora kabisa aliowahi kufanya nao kazi serikalini kutokana na kasi, umahiri na mageuzi mbalimbali ambayo amekuwa akiyafanikisha kwa muda mfupi.

"Kwa kipekee napenda kumpongeza Eliakim Chacha Maswi kwa kuteuliwa kuwa katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na sheria na kwa dhati kabisa naomba nikiri kuwa kupitia utendaji kazi wake mahiri na mzuri, ndugu Maswi amekuwa msaada mkubwa katika kuboresha sekta ya sheria ambapo kwa kipindi kifupi cha takribani miezi tisa tangu ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu amewezesha maboresho mbalimbali kwa Wizara na Taasisi za Wizara na hivyo kuchochea ufanisi katika utendaji kazi na kuimarisha upatikanaji haki kwa wananchi.", alisema Dkt. Ndumbaro.

Dkt. Ndumbaro alibainisha hayo wakati akiwasilisha hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2025/26 huku akieleza kuwa Maboresho mbalimbali yaliyofanywa Ndani ya Wizara na Taasisi zake ni matokeo ya imani kubwa ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kumuamini na kumpa ridhaa ya kutumika kama Katibu Mkuu wa Wizara hiyo.

Pia amemshukuru Maswi na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. Franklin Jasson Rwezimula, akieleza kuwa wamekuwa msaada mkubwa katika kufanikisha shughuli mbalimbali zenye kutekelezwa na Wizara hiyo muhimu kwa ustawi wa utawala wa sheria nchini Tanzania.

> **Naomba nikiri kuwa kupitia utendaji kazi wake mahiri na mzuri, ndugu Maswi amekuwa msaada mkubwa katika kuboresha sekta ya sheria ambapo kwa kipindi kifupi cha takribani miezi tisa tangu ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu amewezesha maboresho mbalimbali kwa Wizara na Taasisi za wizara**









## Nukuu Maridhawa Bajeti 2025/26

Ili kuongeza kasi ya utendaji kazi, mahakama imeendelea kuongeza idadi ya maafisa mahakama ambapo katika mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya majaji10 wameteuliwa na kufikisha idadi ya majai kuwa 146, vilevile mahakimu 91 wameajiriwa hivyo kufanya idadi ya mahakimu kufikia 1426

Kuanzia mwaka 2004 mpaka sasa tumefanya mabadiliko mengi, tumefanya mabadiliko makubwa 15 ikiwa ni pamoja na kufuta sheria ya uchaguzi ya Taifa ya mwaka 1985 na tumefuta sheria ya uchaguzi wa serikali za mitaa ya mwaka 1979, mabadiliko haya yamefanya na bunge hili na linasta

Wizara kupitia Ofisi ya Mwanansheria Mkuu wa Serikali katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 iliandaa miswada ya sheria 16, ilihakiki na kuchapisha sheria ndogo 903 ilinganisha sheria 885 zilizohakikiwa na kuchapishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024

Tumetunga sheria mpya ya uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani Februari 2024 baada ya majadiliano ya muda mrefu na yenye kushirikisha pande zote, tukapata sheria yenye vifungu 168 ikielezea kila jambo linalohusu uchaguzi na kama reforms kubwa tumezifanya Februari 2024, tujiulize tunataka reforms gani na sheria hii haijawahi kutumika",

Bajeti hii sisi tuniita bajeti ya haki, Bajeti ambayo inaenda kumpa haki Mtanzania, kutoa shibe kwa watanzania wenye njaa na kiu ya haki. Italeta mwanga na kuondoa giza la dhuluma ya haki kwa watanzania wanyonge katika kona zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



**Nukuu Maridhawa Bajeti 2025/26**

Kulikuwa na malalamiko ya wakurugenzi kusimamia uchaguzi suala hili limeshapatiwa tiba, sasa hivi uchaguzi utasimamiwa na maafisa waandamizi ambao watateuliwa na tume na kwa njia ya ushindani

Reforms (mabadiliko) yameenda mpaka magereza, sasa wafungwa wataruhuiswa kupiga kura, pia kura ya Rais itaweza kupigwa popote pale sio lazima katika kituo ulichojiandikisha. Tumefanya reforms nyingi tangu mwaka 1961 mpaka leo, tumekuwa na sheria 8 na kanuni 6 tumefuta sheria 2 na tumefanya mabadiliko sheria 6

Dhamana ya kusema kuna uchaguzi au hakuna uchaguzi kwa mujibu wa ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kwa mujibu wa sheria namba 1 na 2 za mwaka 2024 ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi, sio mtu mwingine yeyote, mtu mwingine yeyote anayesema hivyo anajivika joho ambalo sio lake, tuombe watanzania wampuuze

Mwaka uliopita (2024) Mahakama ilipewa kibali cha kuajiri watumishi 522 lakini mwaka huu wamepewa kibali cha kuajiri 1044 kwa mwelekeo huo tunaendelea kupunguza tatizo la upungufu wa wtaumishi wa sekta ya mahakama – **Naibu Waziri Sagini**

Bajeti hii (ya Wizara ya Katiba na Sheria) sasa imepita na tunakwenda sasa kuleta maendeleo na haki kwa Watanzania. Niwaombe taarifa kama hizi za kuwaeleza umma ukweli na kufuta upotoshaji, serikali lazima iwe mstari wa mbele. Katibu Mkuu umepongezwa sana leo nikuombe vipengele vilivyosomwa na Waziri leo viwekwe katika mitandano ya kijamii - **Naibu Spika Zungu**

**Katibu Mkuu,**
**Wizara ya Katiba na Sheria,**
**Mji wa Serikali Mtumba,**
S.L.P. 315 Dodoma.
Masijala: Barua @ sheria.go tz
SIMU: +255 26 2310021
Nukushi: 255 26 2321679
Barua pepe: km@sheria.go.tz
@sheria_Katiba
@katibanasheria_
Wizara ya Katiba na Sheria
Blogu: Katiba Sheria.blogspot.con
Tovuti: www.sheria.go.tz